

MLITOKA KWENDA

KUONA NINI?

 Ikiwa mimi...tulifunga ibada sasa hivi tu, ningesema nimekuwa na wakati mzuri, kusikiliza shuhuda hizi. Na—na nilipoingia na kutazama ile maskani ndogo, jinsi inavyoonekana ya kupendeza, hakuna kisingizio kwa watu, karibu na Utica hapa, kutokuja kanisani. Je, kunacho? Hakika wamefanya vizuri hapa, watu wameweza, kutengeneza mahali pazuri, pa starehe, panapopendeza. Na mahali ambapo sio maridadi sana hata unahisi tu kama wewe—wewe—unajisikia huna starehe, lakini kujisikia tu kweli umestarehe, pazuri tu, safi, nadhifu. Naipenda hiyo kanisani.

² Niliwazia, lile shairi dogo ambalo Ndugu Graham... Yote mawili aliyosoma yalikuwa yana—yanaridhisha kabisa. Unajua, ni... Ni ja—jambo, kwamba wale ambao kwa kawaida wanajaribu kudunisha mtu mwingine, hawa—hawajawahi kushikwa. Vema, mimi ni mmoja wao, Ndugu Graham, amenaswa, mara kadhaa, kwa hiyo ninajua kinachomaanisha.

³ Lakini niliambiwa wakati mmoja, ya kwamba, kule kwa Ballard and Ballard, kuna jamaa aliyeenda kutafuta kazi, wakamwomba asaini jina lake kwenye karatasi. Na alipoenda kusaini jina lake, hakuwa na ninii yoyote... kifutio kwenye mwisho wa penseli.

Yule mtu akamwambia, akasema, “Huna kifutio.”

Akasema, “Naam, sifanyi makosa yoyote.”

⁴ Naye Bw. Ballard akasema, “Basi siwezi kukutumia. Hutafanya chochote.” Hivyo hiyo ni karibu... Nadhani hiyo karibu ni sawa. Ikiwa hatufanyi makosa, hatutakuwa tunafanya chochote. Lakini ninachopenda kuhusu mtu, ni kwamba, unapofanya kosa, askari wa kweli yuko tayari kuinuka na kujaribu tena. Kulikuwa na wimbo mdogo tulioimba.

Nikianguka au nikishindwa, (*kitu kimoja au kingine*)

Acha niinuke na kujaribu tena;

Nisamehe, Bwana,

Na unijaribu mara moja zaidi.

⁵ Niliomba hilo sana, kwa Mungu, mpaka karibu, ninajionea aibu mwenyewe. “Hebu niinuke na kujaribu tena.” Kuanguka mara kwa mara, na kila wakati, mbona, Yeye amekuwa wa rehema kunisaidia kurudi tena.

⁶ Sasa, tukilitazama tu, hakuna saa moja kote katika mchana, hata kidogo, ila ambapo jambo fulani tunalofanya ambalo si sahihi. Na sasa hakuna madogo wala makubwa, yote ni makubwa mbele za Mungu. Kwa hivyo ikiwa ilimbidi Mtume Paulo kufa kila siku, ni zaidi sana jinsi gani tutalazimika kufa kila siku! Unaona?

⁷ Na kisha, nafikiri, mtu ambaye amefanya jambo baya na yuko tayari kulirekebisha, mtazamo halisi wa Kikristo ni kumsamehe mtu huyo. Na hapo ndipo, nafikiri, Ndugu Graham, kwamba watu wa kanisa, leo, wanalikosa sana; badala ya kujaribu kumwinua mtu huyu tena, ni kuendelea tu kuwasukumia mbali zaidi. Unaona? Kama, unaona, Kristo, tulipokuwa chini kabisa, aliinama na kutuinua, na kwa hiyo hilo linatufanya kufikia mahali ambapo tunapaswa kuwa na roho ya namna hiyo, pia.

⁸ Siwezi tu kulitaja jina lake; labda baadhi yenu ndugu mnaweza. Nimekuwa nikiliwazia tangu nilipokuja hapa. Paulo alikuwa... Alikuwa amemkamata mtumwa aliyetoroka. Siwezi kukumbuka jina lake lilikuwa nani, sasa hivi. Hata hivyo, alikuwa na deni kubwa. Na Paulo alikuwa amempenda sana Kristo, hata akatuma habari kwa bwana-mkubwa aliyekuwa anamiliki huyo mtumwa. Alisema, "Sasa amekuwa ndugu mpendwa. Na yote aliyofanya, na yote unayomdai, unaona, yaweke juu yangu. Nami nitakulipa nikija." Unaona, Paulo alikuwa ashakuwa Mkristo, kwa muda mrefu sana, mpaka a—alijua ni nini kusamehe, kilichomaanisha kumsamehe mtu. Alikuwa amesamehewa, yeye mwenyewe. Nami nafikiri kila Mkristo, ambaye amesamehewa kweli, anajua shukrani za msamaha.

⁹ Ndiyo kwanza nisikie ushuhuda wa Ndugu Graham aliotoa kumhusu Ndugu Busty. Huo ni wa Ndugu Rodger... Baba ya Dada Creech. Alifanyiwa upasuaji, siku chache zilizopita, nao wakakuta kansa, nao wakamshona tu. Hivyo basi hebu tuendeleo kumwomba. Lakini moja ya mambo matamu sana... Ndugu Creech alikuwa amenipigia simu, niende na kumwona, nami sikujua alikuwa hospitalini. Ndipo nilipoingia chumbani, akasema, "Ndugu Bill," akasema, "Mara nyingi nimewasikia nyote mkizungumza kuhusu kumwekea mtu mikono."

¹⁰ Nikasema, "Ndiyo, Busty." Nilimwita "Busty." Ni jina lake la utani. Kweli jina lake ni Everett. Nikasema, "Ndiyo."

¹¹ Akasema, "Ninajua tu kwa nini nimekuja hapa." Akasema, "Amekuwa pamoja nami tangu nilipoingia." Akasema, "Na Kitu fulani kiliweka mikono Yake juu yangu, muda mfupi uliopita." Na huko kwenye kona aliona upinde wa mvua. Hapo hapo unajua kuwa Kitu fulani kinapanda juu. Saa imekaribia. Lakini neema ya Mungu kwa hilo... Sisemi hivi kwa sababu ni baba yake Dada Creech. Lakini yeye ni mtu mzuri. Nafikiri

nilimbatiza, miaka iliyopita, katika Jina la Bwana Yesu, lakini hakuwahi kuwa lile tukio halisi lililowekwa wakfu, la kuzaliwa mara ya pili ambalo tunapenda kuona, Ndugu Graham. Hapo ndipo ilipotokea, pale hospitalini. Yeye ni mtu aliyebadilika. Neema ya Mungu, Yule—Yule aliyemtawaza kwa Uzima wa Milele, alitoa upinde wa mvua. Na upinde wa mvua ni agano, akiweka agano Lake naye, naye yuko tayari kwenda. Nina furaha sana kwa ajili ya hilo. Yeye ni mkongwe wa Vita vya Kwanza vya Dunia.

¹² Na muda mfupi uliopita, ama asubuhi ya leo, hasa, niliitwa kwa rafiki yangu wa zamani. Sikuninii... nilikuwa na wakati mgumu kumpata. Wengi wenu mnamkumbuka Bibi Morris, katikati mwa jiji. Ndugu Ruddell amezuru pale tu, muda mfupi uliopita. Naye amepoteza fahamu kwa siku kadhaa. Na yeye anaita tu, kila wakati. Na wakati nilipofika mle ndani, alikuwa akiliita jina langu nilipoingia. Kasema, “Billy ni mvulana mzuri.” Kasema, “Alikuwa na wakati mgumu.” Kasema, “Ni—nilitaka kumwona kabla sijaenda.” Kisha angengoja dakika moja tu, aseme, “Je, mmefanikiwa kumwona? Ni—ninataka kumwona Billy.” Katika dakika chache, alizungumza na mume wake ambaye alikuwa ameondoka, loo, miaka arobaini, hamsini iliyopita, alizungumza naye. Na kuanza kuzungumza na wapendwa wake. Mnajua hiyo inamaanisha nini, kwamba iko karibu tu na Lango.

¹³ Na hilo si ni ajabu? Hata kipofu awezavyo kuwa... Yeye yuko katika ulimwengu wa giza. Ana umri wa miaka tisini, moja kwa moja kwenye tisini, kama themanini na tisa, hivi. Na sasa, bado, macho yake yako karibu sana na upande ule mwingine, mpaka anaweza kuona vi—vitu vilivyo upande ule mwingine, na huwezi kuviona upande huu. Je, uliwahi kuwazia hilo? Kumtazama mpendwa, wanapofika mwisho wa safari? Waangalie.

¹⁴ Mzee Ndugu Bosworth, mshiriki wangu wa zamani, nilikimbilia huko Florida, kumwona, mimi na Meda, yapata miaka miwili iliyopita, alipokuwa akifa, karibu ti... themanini na kitu, themanini na nne, naamini. Alikuwa ametoka tu Afrika pamoja nami, kwenye mkutano. Mzee huyu mtauwa amelala hapo, kwenye maskini kona fulani. Niliingia ndani, mimi... Hiyo mikono midogo mizee ilininyooshea, askari mkongwe wa yapata miaka sabini ya kuhubiri. Ndipo nikamshika mikononi mwangu namna *hiyo*. Nikapaza sauti, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake.”

¹⁵ Nami nikaketi kando ya kitanda pamoja naye, nikaweka kichwa chake juu ya bega langu. Mimi... Alikuwa kidogo akinipapasa. Akasema, “Mwanangu,” kasema, “usishindwe. Yaingie maeneo hayo, upesi, maana hatuna muda mwingi.”

Nikasema, “Unatambua kuwa unaenda?”

¹⁶ Akasema, “Ndiyo. Ninaenda, hivi karibuni tu.” Akasema, “Ninataka kukuambia jambo fulani, Ndugu Branham, huu ndio wakati wa furaha kuliko wote katika maisha yangu yote.”

¹⁷ Nami nikasema, “Kwa nini useme hivyo, Ndugu Bosworth, nawe una—unakufa?”

¹⁸ “Kwa nini,” akasema, “dakika yoyote, ninamtazamia Yeye aingie mlangoni, anichukue, Yule ambaye nimempenda miaka hii yote.” Mimi... Tulinwacha yeye, mimi na mke wangu, na kisha tuliporudi... .

¹⁹ Yapata saa moja au mbili kabla hajafa... Alikuwa amelala, akaamka, akatazama chumbani. Akasema, “Baba!” Akanyanyuka kwa nguvu zake na kupeana mikono na baba yake, na mama yake. Akasema, “Huyu hapa Ndugu John. Uliongoka katika mkutano wangu, miaka hamsini iliyopita. Huyu hapa *nanii*.” Akapeana mikono na waongofo wake ambao walikuwa wameondoka kwa miaka na miaka.

²⁰ Nini kinatokea basi, rafiki? Nafikiri hatutambui tu kwamba haya yanahusu nini. Wakati mwingine ninashangaa, hata tunapokuja kwenye mkutano, kuabudu, kama hatuna, namna fulani ya maoni yasiyofaa, kufikiri kwamba tunakuja tu kukutana pamoja. Hiyo ni nzuri. Ina madhumuni yake. Au, kufurahi na kuwa na wakati mzuri, hiyo ina kusudi lake. Lakini tuko kwenye maandalizi. Tunajiandaa kwa ajili ya kitu fulani.

²¹ Na nimesema hivi mara kadhaa. Inaweza kuwa vizuri kuifanya tena. Ninapoanza kuzeeka, na kuanza kuona kwamba siku zangu zinapungua, ninaanza kuwazia maisha haya kwa njia fulani, Ndugu Graham, kana kwamba ilikuwa—ilikuwa ni ndoto mbaya nimekuwa nayo. Wengi wetu hapa tumeota, na tumeota ndoto nzito. Unajaribu kujipiga mwenyewe. Wengi wenu mmefanya hivyo. Nimefanya, mara nyingi. Kujaribu kujiamsha mwenyewe, kwa njia fulani unajua kwamba umelala.

²² Na ninahisi hiyo ni kama maisha yalivyo. Wakati tu tunapofikiria tumenyooka, na kila kitu kitakuwa sawa, basi kitu fulani kinakuja na kukiondoa tena. Sasa, ninyi watu wote, ambao ni wa karibu umri wangu hasa, mnajua jambo hilo. Majaribu na vita vya maisha! Kwa hivyo wakati mwingine ninajaribu kujiamsha, “Ee Bwana!” Na moja ya asubuhi hizi, ama moja ya jioni hizi, ama wakati fulani, nitaamka. Nitakuwa katika Uwepo Wake. Kisha majaribu yote na huzuni zote zitakwisha. Natumai hiyo ni kweli. Natumaini kwamba siku moja ninaweza kuamka kuwa kama Yeye. Hiyo ndiyo shauku ya moyo wangu, ni kuamka katika mfano Wake, kumwona Yeye.

²³ Na, kama Paulo alivyosema, sasa kuna jambo moja ambalo ninataka kulihakikisha, ninapoweza, katika akili yangu timamu. Nataka kuhakikisha, kwamba, “Ninamjua katika Nguvu za kufufuka Kwake,” haijalishi ni nini kingine kinachotokea. Nikifa maskini, na wanizike katika shamba la

mfinyanzi, au kaburi langu litakuwa chini ya mto au bahari, popote litakapokuwa, nataka kujua jambo moja. Nataka kumjua Yeye. Hayo ndiyo yote yanayojalisha sasa, hiyo ni kweli, kumjua Yeye katika Nguvu za kufufuka Kwake.

²⁴ Kwa maana najua hili, kuna mlango mkubwa sana uliowekwa mbele yangu, nao unaitwa *mauti*, na iko mbele ya kila mmoja wetu. Na kila wakati moyo wetu unapopiga, tunakuwa pigo moja karibu zaidi na mlango huo. Hautapiga tena pigo hilo. Tuko pigo moja karibu zaidi, na moja ya siku hizi tunakuja kwenye mlango huo. Unaitwa *kifo*, na kila mmoja wetu atakutana nao. Na nikifika huko, hakika sitaki kuingia mle kama mwoga. Ninataka kuingia mle ndani nikiwa nimejivika mavazi Yake, na neema Yake. Nikijua jambo hili moja, ya kwamba, atakapoita, nitatoka kule, siku moja. Hilo ndilo ninaloishia, leo, ni kufanya hivyo, kumjua Yeye na kumtumikia.

²⁵ Na wahudumu hawa wachanga hapa, Ndugu Graham, na kama Ndugu Ruddell na hao wengine, hakika ninawasihi washikilie, waendeleo kukaza mwendo. Nilipoingia usiku wa leo na kuketi kule nyuma na kuzisikia hizo nyimbo, wakiimba tu. . . wanapopiga makofi, kama vile *Njoo Ule*. Mbona, ningeweza kumwona Dada Snelling, vizuri tu, amesimama pale, akipiga makofi, kitu kama hicho, akiimba, “Njoo ule. Bwana anaita, ‘Njoo ule.’” Vivyo hivyo, na kuwaona wale watakatifu wote wa zamani ambao wameondoka. Vema, wanangojea tu ng’ambo ya mpaka huko. Na mimi—mimi—mimi—mimi ninataka kuwaona, moja ya siku hizi, mama mzee, Pugh. Ninaweza kumwona Shangazi Noan amesimama pale mlangoni, wakati huo alipokuwa vibaya sana. Nilikuja nikitembea, mimi na Ndugu George, tukasema, “Vema, kuna ufufuo mmoja wa wafu,” kasema, “Mimi ndiye mtu huyo.” Ninaweza tu kumwona dhahiri kabisa, Dada Weber na hao wengine wote.

²⁶ Sema, jambo jingine, nadhani Frankie anaendelea vizuri sana sasa hivi. Nilimpigia simu, masafia marefu, hivi majuzi usiku, nikaomba pamoja naye tena. Akasema—kasema, “Hii ndiyo mara ya kwanza nilipohisi mguso wa Mungu kwa miaka mingi.” Akasema, “Nitafanya ziara yangu kwenye maskani, moja ya mambo ya kwanza, mara nirudipo Indiana, nirudi hapa chini.” Kwa hiyo, Bwana asifiwe. Frankie ni mvulana mzuri, mvulana mzuri. Amekuwa na shida zake. Don hayupo hapa, sivyo? Ndiyo. Sikufikiri, hapa. Lakini yeye—yeye amekuwa na shida zake, lakini Mungu atamwondoa jukwaani, moja ya siku hizi, ikiwa hatakuja. Kwa hiyo, hebu tumwombe.

Kabla hatujafungua Neno, na tuinamishe vichwa vyetu kwa Mwandishi.

²⁷ Ee Roho Mtakatifu wa Mungu uliye mkuu, maisha yanapoanza, maisha haya yapatikanayo na mauti yanaanza kuwa na mvi, na kukunja uso, tunaweza kuhisi mtetemo huo

wa Uzima wa Milele ndani ya maisha yetu yanayokufa, na unavimba kwenye koo zetu. Tunapojua ya kwamba kama si Wewe, kwamba, mara tu maisha haya yanapokwisha, yote yangekwisha. Lakini, kama Paulo wa kale alivyosema, “Ashukuriwe Mungu atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Mauti hayakuweza kumchoma, wala kaburi halikuweza kumshikilia. Na mavumbi ya mwili huo mtakatifu yanangoja ufufuo, usiku wa leo, bali nafsi yake iko katika Uwepo wa Kristo, ambaye alisema, “Ilikuwa bora zaidi kuachana, kuliko kuwa pamoja.”

28 Na ile Injili kuu ambayo aliitangaza kwa ujasiri katika siku zake, hata kutoka nyuma ya nondo za gerezani, aliandika wakati macho yake yalikuwa yanamsumbua vibaya sana mpaka akaandika kwa herufi kubwa sana. Na alikuwa amepigana na wanyama, na alikuwa na mapigo mengi juu ya mwili wake. Injili hiyo hiyo tukufu, tunashindana na yote yaliyo ndani yetu, kuifanya iendelee hadi siku hiyo.

29 Tunashukuru kwa ajili ya maskani hii ndogo, kwa ajili ya mchungaji wake, washiriki wake, halmashauri yote, na kwa ajili ya mji mdogo uliomo; kwani kwa kweli, Bwana, hapa ndipo nilipohubiri mahubiri yangu ya kwanza. Nami naomba, Ee Bwana, kwamba kanisa hili dogo na roho ya kulijenga vitabaki hadi Kuja kwake Bwana Yesu, na ya kwamba wote walio washiriki hapa, na wanakuja hapa, hakutakuwa na hata mmoja wao atakayepotea. Ninaombea uamsho mkubwa wa kiroho hapa Utica. Jalia Nguvu za Yesu Kristo zienee katika mji huu mdogo na kuwaita wengi kwa Kristo. Wabariki wote wanaohusika katika mambo haya, Bwana.

30 Tungeomba ya kwamba Roho Mtakatifu aseme nasi, usiku wa leo. Wape huo mkutano mkuu, Jumapili, ambao wanatazamia. Na iwe tukufu kwa Uwepo Wako.

31 Utusamehe dhambi zetu. Na kama kukiwepo na mmoja miongoni mwetu, ambaye hakujui Wewe usiku wa leo, tumaini hili la neema halidundi chini ya vifua vyao, basi jalia walipate usiku wa leo, Bwana, vile visima vikubwa vya furaha vinavyobubujika kuingia Uzima wa Milele. Sikia maombi yetu manyenyekevu.

32 Bariiki usomaji wa Neno. Na jalia Roho ayachukue Maneno na kuyapanda mahali ambapo yangefanya mema zaidi. Kwa maana tunaomba katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

33 Unajua, ninapokuja Utica, haionekani kama kuja hapa kuhubiri. Inaonekana tu kama kuja hapa kuzungumza na watu kwa muda kidogo, maana ninawajua ninyi nyote, na ushirika mdogo tu.

34 Sasa hebu na tusome, usiku wa leo, kutoka kwenye Mathayo sura ya 11, aya chache, hadi yapata ya 15.

³⁵ Ninapenda kusoma Neno Lake, kwa sababu Neno Lake ni kweli na ni la Milele. Sasa, sababu napenda kusoma Neno Lake, kwa sababu maneno yangu yatashindwa, mimi ni mwanadamu, lakini Maneno Yake hayawezi kushindwa kamwe. Na kwenu ninyi watu wa thamani mlio hapa, usiku wa leo, najua kama si zaidi ya kusoma Neno hili, utapata kitu fulani, utaenda nyumbani, kwa maana hiki ndicho Chakula ambacho Ndugu Graham alikuwa akizungumzia. Na hebu Yeye atuhuishie Hilo, tunaposoma.

Ikawa, Yesu alipokwisha kuwaagiza wanafunzi wake kumi na wawili, alitoka huko na kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao.

Naye Yohana aliposikia kule gerezani matendo yake Kristo, aliwatuma wawili wa wanafunzi wake,

Wakamwuliza, Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?

Yesu akajibu akawaambia, Nendeni mkamweleze Yohana tena haya mnayoyasikia na kuyaona;

Vipofu wanapata kuona, . . . viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa, na viziwi wanasikia, na wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema.

Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami.

Na hao walipokwenda zao, Yesu alianza kuwaambia makutano habari za Yohana, Mlitoka kwenda nyikani kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na . . . upepo?

Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo? tazama, watu wavaao mavazi mororo wamo katika nyumba za wafalme.

Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Nabii? naam, nawaambia, na aliye mkuu zaidi ya nabii.

Kwa maana huyu ndiye, . . . aliyeandikiwa haya, Tazama, namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakayeitengeneza njia yako mbele yako.

Amin, nawaambia, Hajaondokea mtu katika wale waliozaliwa na mwanamke aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye.

Na tangu siku hiyo, siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, na wenye nguvu huuteka kwa nguvu.

Kwa maana manabii wote na . . . torati walitabiri mpaka wakati wa Yohana.

Na ikiwa mnataka kukubali, yeye ndiye Eliya, atakayekuja.

Mwenye sikio ya kusikia, na asikie.

³⁶ Kama nikijaribu kuchukua kifungu kidogo, kwa hotuba, kwa muktadha wa somo hili, ningechukua hili: *Mlitoka Kwenda Kuona Nini?*

³⁷ Yohana, katika siku zake, na ulimwengu, alichukuliwa kuwa mtu wa porini. Alikuwa nusu uchi, amejifunika kipande cha ngozi ya kondoo, na ndevu zilizosokotana usoni mwake, na labda nywele zake zilisimama kutoka upande. Na kwa . . . ulimwengu tu, watu huko nje ulimwenguni, yeye alikuwa mtu wa mwituni. Tungemwita “mwenye kichaa,” ni mchungaji mzee tu aliyeishi nyikani.

³⁸ Kwa kanisa, kwa kuwa alihubiri, alikuwa mshupavu. Kanisa lilifikiri, “Mtu huyo kabisa, kwa hakika, ni mwenye kichaa wa kidini.” Kama angekuwa, leo, angalifikiriwa leo hii kama ilivyokuwa wakati huo, kwa sababu ulimwengu haubadiliki. Watu wanakuja, na vizazi vipya vinainuka, lakini roho inayotawala ulimwengu, ni kama tu ilivyokuwa wakati huo. Na itakuwa, mradi tu kuna ulimwengu.

³⁹ Lakini wale waliomjua Yohana, wale waliomwamini, walitoka kwenda kuona kitu ambacho kilikuwa halisi.

⁴⁰ Huko inagawanyika, leo, kama ilivyokuwa wakati huo, katika matabaka matatu tofauti: ulimwengu, kanisa, na mwaminio halisi, wa kweli. Hivyo ndivyo ulimwengu unavyosimama leo: ulimwengu, asiyeamini; kanisa, mshiriki vuguvugu; na kisha mwaminio halisi, wa kweli. Baadhi ya watu huenda makanisani kutafuta makosa katika kanisa hilo. Na baadhi ya watu huenda nje kuwa na hadhi ya kijamii, ama kile ambacho wangefikiria kuwa tabaka bora zaidi, ama kujumuika pamoja. Wengine huenda kutafuta amani, kwenda kumtafuta Mungu katika kitu halisi. Huyo ndiye anayepata manufaa ya mkutano. Daima nimesema kwamba Injili huzaa aina tatu za watu: asiyeamini, mwamini wa kujifanya, na mwamini. Na daima imekuwa hivyo. Inategemea tu kile unachoenda, mtazamo ulio nao.

⁴¹ Ujumbe aliohubiri, mbona, ulimwengu haungetoka kwenda kusikia Ujumbe kama huo. Wangeuhukumu, leo, kama tu walivyofanya wakati huo. Jambo lile lile, kama Ujumbe ule ule ungehubiriwa.

⁴² Lakini bila shaka haukuwa Ujumbe mbaya sana. Yesu alisema, “Hapakuwa na mtu aliyepata kuzaliwa, mpaka wakati huo, aliyekuwa mkuu kama Yohana Mbatizaji.” Yesu aliidhinisha Ujumbe wake. Alisema, “Je, ulienda kusikia upepo unaotikisa nyasi, unainama tu kwa kila kitu? Si Yohana.” Akasema, “Basi ulikwenda kumwona mtu aliyevaa mavazi mazuri?” Akasema, “Nawaambia, wale wanaovaa mavazi mazuri ni wa majumba ya wafalme. Lakini,” akasema, “mlienda kuona nini basi, nabii? Nawaambieni, Yohana alikuwa zaidi ya

nabii. Kwa maana huyu ndiye aliyetabiriwa, au aliyebashiriwa, ya kwamba, ‘Angetengeneza njia mbele ya uso Wako.’”

Mtu mashuhuri, Yohana, lakini ulimwengu haungeweza kuiona hivyo.

⁴³ Ilikuwa ni nini juu ya Yohana ambacho kilivutia umakini? Kwa baadhi yao walikwenda kumwona mtu wa mwituni, akizungusha mikono yake, nusu uchi, nywele mwilini mwake mwote. Alikuwa mtu aliyeonekana wa kutisha, labda mikono yake, mikono, maana yeye alikuwa ni mfano mkamilifu wa Eliya, na Eliya alikuwa mtu aliyejaa nywele.

⁴⁴ Nao wakaenda kumwona. Baadhi yao walikwenda kumwona, ili tu kuona jinsi alivyoonekana. Wengine walikwenda kuona, ili kutokubaliana naye. Wengine walikwenda kuona, ili kuona ni faida gani wangeweza kupata kutoka kwayo. Ndivyo ingekuwa leo ikiwa atakuja. Kama angalikuwa hapa leo ama Ujumbe wake ungeendelezwa kama ulivyokuwa wakati huo, lingekuwa ni jambo lile lile. Sasa hebu...

⁴⁵ Kama Ujumbe wake ulikuwa wa kudumaza sana, basi, hata ulitikisa maeneo, hebu tuone kile alichohubiri. Jambo la kwanza alilohubiri lilikuwa ni toba kwa wote.

⁴⁶ Na toba kila mara hupofusha macho ya asiyeamini, au mshiriki wa kanisa. Mshiriki wa kanisa anahisi kwamba hana kitu cha kutubu. Na wakati mtu huyo, au watu, wanapofikia mahali pale unapofikiri huna chochote cha kutubu, uko katika hali mbaya zaidi, ingawa ni m—m—mshiriki wa kanisa, uko katika hali mbaya zaidi kuliko mwenye dhambi mtaani.

⁴⁷ Kwa maana, Maandiko yalisema, katika Kitabu cha Ufunuo, yakizungumza juu ya kanisa, yalisema, “Alikuwa uchi, mnyonge, mwenye mashaka, na kipofu, wala hakujua.”

⁴⁸ Sasa, kama mtu angekuwako barabarani, na alikuwa kipofu, hilo lingekuwa jambo baya sana. Ikiwa angekuwa maskini, lingekuwa baya. Uchi; baya sana. Lakini, bila kujua, hiyo ndiyo sehemu ya kusikitisha. Na kuna watu, leo, wanaodai kuwa Wakristo, ambao ni wa kanisa, ambao hawajui kwamba wanahitaji toba. Na kumwambia mtu hivyo, kunawakoroga.

⁴⁹ Sasa, wakati Yohana alipoanza kuhubiri toba kwa watu hao wa kanisa, walisema, “Angalia hapa. Tunaye Ibrahimu baba yetu. Hatuhitaji hata mmoja wa wahubiri hawa wa porini wanaotoka nyikani. Makundi haya yasiyo na elimu, yasiyo ya madhehebu. Hatuhitaji kupiga kelele kwao na kuendelea, kwa maana tunaye Ibrahimu ndiye baba yetu.”

⁵⁰ Vivyo hivyo na Ujumbe huo huo ungepofusha kanisa siku hizi. Kama ungeuliza mtu, haraka, “Je, wewe ni Mkristo?”

Sema, “Ndiyo.”

51 Upesi watasema, “Je wewe ni wa dhehebu gani?” Sasa, hiyo ni sawa, lakini haina uhusiano wowote na Ukristo.

52 Mmoja wao atasema, “Vema, mimi ni Mmethodisti, ama Mbaptisti, au Mpresbiteri,” au kanisa lolote ambalo wanahusiana nalo. Ambalo ni sawa kabisa, lakini hilo halijibu swali. Bado unahitaji toba, na toba huwatikisa watu. Wanafikiri hawaihitaji.

53 “Mimi—mimi ndiye shemasi. Mimi...ninafanya mambo fulani ka—kanisani.” Hiyo haileti udhuru wowote. Bado unahitaji toba.

54 Na Yohana alikuwa akithibitisha tu ahadi ya Mungu na kuhubiri dhidi ya dini ya kiakili. Na ikiwa yuko... Ujumbe huo huo umetolewa, leo, ingeongeza kiasi cha m—mtafaruku miongoni mwa watu wa dini kama ilivyokuwa wakati huo. Maana, tofauti pekee wanayosema, “Kwa kuwa tunaye baba yetu Ibrahimu,” wanasema, leo, “Vema, nataka ujue, mimi ni mshiriki wa kusanyiko *fulani-fulani*.”

55 Naye Yohana akasema, “Lakini shoka limewekwa kwenye shina la mti, na kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.” Naye akasema, “Anakuja na kipepeto mkononi Mwake, na atasafisha kabisa uwanda, na kuchoma makapi, na kukusanya ngano kwenye ghala.”

56 Loo, si ajabu Yesu alisema, “Hakukuwa na mtu aliyezaliwa kama yeye.” Na sababu ya Yohana kufanya hivi, alikuwa mtu maalum. Mungu humhamasisha mtu, humhamasisha kwa nyenzo Zake Mwenyewe. Hawakwenda nyikani kusikiliza hotuba ya kiakili, kitu ambacho kingekuwa kama hotuba ya mwanasiasa. Yesu alisema, “Mlienda kusikia nini mlipotoka?” Wakati watu waliomsikia Yohana, walimsikia mtu aliyezaliwa, tangu tumboni mwa mama yake, amejaa Roho Mtakatifu. Hawakusikia mtu wa kupatana juu ya Injili. Hawakusikia madhehebu yakibishana, “*Huyu* yuko sahihi, na *yule* yuko makosani.” Walisikia Ujumbe wa Injili uliochoma moyo.

57 Yohana alihubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hakuwahi kuhubiri kitu ambacho hakuwa nacho. Alihubiri kile alichokuwa amepokea.

58 Na watu wa Mungu waliotumwa hudumani, leo, hawana haki ya kuhubiri Injili, bila ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sifa ya kwanza ya mhudumu, ni kujazwa na Roho Mtakatifu.

59 “Kwa hivyo mlienda kuona nini? Mtu aliyevaa mavazi mororo?” Akasema, “Wale waliovaa mavazi mororo ni wa majumba ya wafalme.” Yohana alikuwa mbali sana na Hollywood, kuwa mhubiri aliyevalia kijamii.

“Mlikwenda kusikia nini? Mwanaume mwenye elimu nzuri?”

⁶⁰ Yohana alienda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa, historia inasema. Elimu yake ilitoka kwa Mungu. Mbona, walienda kumwona meneja wake wa kampeni, mnenaji hodari ambaye angeweza kuandaa kampeni na kufanya makanisa yote kushirikiana? Mbona, bila shaka sivyo. Aliwakemea Mafarisayo na Masadukayo. Aliita muungano wa wahudumu “kundi la nyoka.” Alisema, “Loo, enyi nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia ghadhabu inayokuja? Msianze kusema ndani yenu, ‘Sisi ni wa *hili*, au sisi ni wa *lile*,’ kwa maana Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Tunachohitaji leo ni mahubiri zaidi ya Yohana Mbatizaji, yaliyopakwa mafuta na Roho Mtakatifu. Na hakughairi, walipoona alipohubiri juu ya ndoa na talaka. Alihubiri moja kwa moja, kwenye Injili iliyonyooka, kwa sababu hakuighairi. Kwa nini? Alipakwa mafuta. Asingeweza kujizuia kuwa kile alichokuwa.

⁶¹ Huwezi kujizuia kuwa kile ulicho. Hata kama wewe ni mwenye dhambi, huwajibiki kwa kuwa mwenye dhambi. Unawajibika kwa kubaki mwenye dhambi. Kuna njia iliyoandaliwa kwa ajili yako. Lakini kuwa mwenye dhambi, ulizaliwa hivyo. Mungu hakupeleki kuzimu kwa kuwa mwenye dhambi. Mungu anakupeleka kuzimu kwa sababu hutatubu na kumchukua Kristo kama Mwokozi wako. Unakataa kuchukua njia sahihi. Unajituma mwenyewe matesoni. Unaituma nafsi yako mwenyewe kwenye hatima yake ya Milele, juu ya hiari ya kujiamulia ya imani yako mwenyewe. Mungu hampeleki mtu yeyote kuzimuni. Hajawahi kufanya na hatawahi. Watu hujipeleka wenyewe kuzimuni kwa sababu wanakataa ku—kuikubali njia ya wokovu. Mungu sio... Yeye ni mvumilivu. Hataki yeyote aangamie; kamwe hakutaka.

⁶² Bali watu heri waenende gizani kuliko kuenenda Nuruni. Sababu yake ni kwamba, wameninii... Wamezaliwa katika hali hiyo, na hawana hamu yoyote kuichukua Nuru. Na wajumbe wakaja, kutoka mashariki na magharibi, na kaskazini na kusini, na kutupa viziwi. Huduma ya nyimbo, shuhuda, mahubiri, katika njia ya mwenye dhambi, na kwa makusudi anapitia moja kwa moja kati yao na kisha kusema kwamba Mungu anawajibika au ana hatia. Mungu ni mwema na mwingi wa rehema. Na asingependa mtu yeyote apotee. Lakini mwanadamu anataka kupotea kwa sababu ni tamaa yake. Anakataa kutembea katika Nuru, hiyo ndiyo inayomfanya apotee. Sawa.

⁶³ Sasa, Yohana, alikuwa anapinga mahubiri haya ya kiakili. Hakuwa na elimu, kwa hivyo hangeweza kupata ushirikiano.

⁶⁴ Nadhani, hata katika jiji la ukubwa huu, kama Ndugu Graham angejaribu kusema, “Sasa tutakuwa na uamsho hapa, na tutaenda kote mjini...” Niliona wakati alipokuwa na uamsho wake, kwamba, kwenye njia panda, ishara ndogo, ilisema, “Uamsho huko Utica.” Haikusema ni kanisa gani.

Ilisema tu, “Kuna uamsho unaendelea. Njoni. Kila mtu amekaribishwa.” Nafikiri, kama angeenda kutoka kwa mhubiri hadi kwa mhubiri, kote nchini hapa, angekuwa na wakati mgumu kupata ushirikiano kamili. Asingefanya hivyo.

⁶⁵ Kama nikija hapa kufanya kampeni pamoja naye, Ndugu Beeler na Ndugu Ruddell, na sisi sote pamoja, tulikusanyika kufanya kampeni huko Jeffersonville au New Albany, ama mahali fulani, ingetubidi—ingetubidi tuvute umati kwa mahubiri yetu wenyewe, na kwa Roho Mtakatifu. Makanisa yangesema, “Naam, hatuna uhusiano wowote na hilo. Wanatoka seminari gani? Wanaungwa mkono kutoka wapi?”

⁶⁶ Sifa zetu, kama Yohana angesema, “Haitoki kwenu Mafarisayo. Mungu aliniita kuhubiri Injili. Hiyo ndiyo sifa yangu.” Watu wote waliotumwa na Mungu wanasimama kwenye misingi ile ile. Kanisa halikupeleki. Mungu hutuma mtu aliyetumwa na Mungu. Naye Yohana alikuwa wa aina hiyo.

⁶⁷ Yesu alisema, “Mlitoka kwenda kuona nini? Je, mlienda kuona Fa—Farisayo, au Msadukayo? Mmethodisti, ama Mbaptisti, au Mpresbiteri? Mlikwenda kuona nini? Je, alikuwa amevalia vizuri? Alikuwa—alikuwa na ufasaha katika hotuba yake?”

⁶⁸ Alifanya nini zaidi ya kusimama pale na kukemea kila jambo lililokuwa baya! Hata yule mkuu wa mkoa akatoka kwenda kumwona, ambaye ni gavana wa jimbo; akatoka nje huko, akiishi na mke wa kaka yake mwenyewe. Yohana akamwendea na kusema, “Si halali kwako kuwa naye.” Ndiyo!

⁶⁹ “Mlikwenda kuona nini? Je, mlienda kumwona mhubiri wa kimadhehebu? Je, mlienda kuona mzungumzaji wa kiakili?”

⁷⁰ Mbona, leo, hilo lingekuwa mbali na kile ulimwengu ungetaka leo. Mbona, wanataka kitu ambacho ni fasaha; mahema na bendera kubwa, maarufu, ama Daktari fulani mkuu wa Uungu; makanisa yote yakishirikiana, watu wasomi wakitangulia, mazungumzo ya kiakili.

⁷¹ Lakini unapomwona mtu wa Mungu, kwa kawaida huwa yuko nje kwenye uchochoro mahali fulani, amesimama barabarani, ama jengo fulani dogo, akihubiri Injili isiyoghoshiwa ya Yesu Kristo. Huyo ndiye mtu ambaye Mungu alimtuma, ndugu, akiweka shoka kwenye shina la mti, akihubiri Injili bila kujali watu wanafikiri nini kuihusu. Anasimama peke yake!

⁷² “Mlitoka kwenda kuona nini, mtu mwenye elimu nyingi?” Hakika siyo, hakuwa na yoyote. Alienda nyikani, akiwa na umri wa miaka tisa. Akatoka, akiwa na umri wa miaka thelathini.

⁷³ Akihubiri toba! Akiwakemea Mafarisayo! Kwa nini alifanya hivyo? Hakuweza kujizuia kuwa kile alichokuwa. Roho ya Eliya ilikuwa juu yake. Hakuweza kujizuia kwa sababu alivaa nguo

kama alivyofanya. Asili yake ilikuwa hivyo. Hangeweza kujizuia kuhubiri juu ya wanawake kutembea ovyoovyo, kwa maana Roho wa Eliya alikuwa juu yake. Alikuwa kile alichokuwa. Alimwambia Herodia, akamkemea, usoni pake. Aliwaambia watu kile alichofikiri. Kwa nini, hakuweza kujizuia. Huo ulikuwa upako wake. Alikuwa ni Eliya.

⁷⁴ Kisha ikiwa mwanamume au mwanamke... Upako wako unaonekana juu yako. Chochote roho yako ilicho, inakusukuma. Unasukumwa na roho. Na kama Roho wa Yesu Kristo yuko juu ya Mkristo, mwaminio, si ajabu yeye ni mtu wa kipekee. Si ajabu, kuna Kitu kinachotembea ndani yake. Wito wa Mungu uko ndani yake. Roho wa Kristo anamsukuma, na inambidi kuenenda jinsi Roho anavyomsukuma.

⁷⁵ Je, ungeweza kuwazia kumwona Yohana akishuka chini pale, aseme, “Loo, *hiyo* ni sawa. *Hii* ni sawa.” Maadamu Roho wa Eliya alikuwa juu yake, alitenda kama Eliya.

⁷⁶ Unapochukua watu hawa wanaoenda sasa, huanza na kusema, “Loo, nitakuwa Mkristo,” na wanaanza vizuri. Jambo la kwanza, kama miezi sita, wanaanza kurudi nyuma. Wanaanza *hivi, vile*. Unaweza kutambua papo hapo kwamba upako unawaacha. Kwa maana maadamu Roho wa Kristo yu ndani yako, atakufanya kuwa kama Kristo.

⁷⁷ Sasa watu wengi wana maoni yasiyo sahihi juu ya Kristo. Baadhi ya watu wanafikiri kwamba Kristo alikuwa dondoadume. Kristo alikuwa ndiye mkuu kuliko watu wote. Alikuwa ndiye mtu wa mfano. Sio tu kwamba alikuwa mwanadamu, bali alikuwa Mungu-Mwanadamu. Alikuwa “Mungu pamoja nasi; Imanueli.” Alikuwa mnyenyekevu kuliko watu wote. Lakini, unaweza kuwa mnyenyekevu sana, unaweza kuwa mnyenyekevu sana mpaka ibilisi angekufanya kikaragosi. Alikuwa mnyenyekevu vya kutosha kutawadha miguu ya wanafunzi. Alikuwa anasamehe vya kutosha kuwaombea wale walioingiza miiba mikononi Mwake. Lakini alikuwa Mwanadamu vya kutosha kusuka kamba na kuwafukuza wabadilisha pesa kutoka kwa nyumba.

⁷⁸ Ndiyo, Yohana alikuwa mwanadamu vya kutosha kuwa mpole na mnyenyekevu. Alikuwa mwanadamu vya kutosha kusimama kwenye kingo za Yordani. Hakuhitaji sinagogi kubwa au mahali pa kuhubiri. Alikuwa mnyenyekevu. Alichukua anga angavu za samawati. Alikuwa mnyenyekevu vya kutosha hivi kwamba hakuwaita watu kulazimika kuwa na pesa nyingi sana, kuchunga kanisa lao.

⁷⁹ Alikula panzi na asali ya mwituni, nzige. Katika nchi hiyo, wanawatia koponi. Ni panzi wakubwa, warefu; kuwatengeneza kwa achali, kuwachoma, kila njia nyingine, ili kuwala. Hao ndio alioishia. Na vazi lake lilikuwa ni kipande cha ngozi ya kondoo alichojifunika.

80 Yesu alisema, “Mlienda kuona nini? Mlienda kuona nini? Mtu ambaye angekubaliana na Mafarisayo; unyasi unaotikiswa na kila upepo? Anayeingia na Masadukayo wanapoingia? Siku moja yuko *hivi*, na siku nyingine yuko *vile*”? Kasema, “Hamkwenda kuona kitu kama hicho.” Kasema, “Mlienda kuona mtu aliyevalia vizuri? Hapana. Msomi? Hapana. Mlikwenda kuona nini?”

81 Akasema, “Nendeni mkamwonyeshe Yohana kinachoendelea hapa. Viwete wanatembea. Vipofu wanaona. Viziwi wanasikia. Wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa Injili. Heri mtu yule asiyechukizwa Nami.” Loo, jamani! Hiyo ilikuwa ni ishara ya Masihi. Hiyo ilikuwa ni ishara ya kumwonyesha.

82 Hiyo ndiyo ishara kwamba kanisa la kweli la utakatifu leo, ingawa yanaanguka, lingali ndilo alama ya mwito wa Yesu Kristo. Wanaume na wanawake wanaosimama kwa ajili ya Injili isiyoghoshiwa, ya wokovu kwa nafsi, kwa maskini, kwa wahitaji. Si kundi la watu wa kiserikali ambao wamevaa makanisani mwao hivi kwamba mtu maskini anahisi hafai, bali kundi la watu wanyenyekevu. Hapo ndipo Injili inapohubiriwa. Wagonjwa wanapona. Wanaombea wagonjwa. Mungu huthibitisha huduma yao kwa ishara na maajabu. Hiyo hapo Injili inahubiriwa kwa maskini.

“Nenda kamuonyeshe Yohana mambo haya.” Loo, jamani!

83 Jinsi ambavyo Mungu alimchukua mtu huyo bila elimu; alimchukua mtu huyo bila suti moja ya nguo ya kuvaa; akamchukua mtu huyo bila vazi la kuweka juu ya mabega yake; mtu ambaye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake; mtu ambaye hakuwa na chakula kizuri cha kuketi karibu; na kuyashtua mataifa naye.

84 Haleluya! Rehema! Ninapowazia hilo, huniamsha kwa jambo fulani. Je, ni lazima tufanye? Nilimwambia mke wangu, hivi majuzi, “Mpenzi, nina umri wa miaka hamsini. Siwezi kuwa hapa kwa muda mrefu sana.”

85 Kisha nikatoka nje. Nilisimama pale msituni. Nilienda kuwinda. Nilisimama pale mwituni kidogo. Niliwazia hilo, “Umri wa miaka hamsini. Kuna nini?”

86 Kisha Kitu fulani kikasema, kuniambia, “Mungu angeweza kukufundisha kwa miaka hamsini, kufanya kazi ya dakika hamsini.” Chochote mafunzo yamekuwa, Mungu anajua anachofanya. Alimfundisha Musa miaka themanini, kupata miaka arobaini ya utumishi kutoka kwake. Mungu anawafundisha watu wake. Mungu analifundisha Kanisa Lake. Ikiwa tuko tayari kumwacha Mungu awe na njia Yake, na ku—kufanya jambo ambalo ni sahihi. Ikiwa tuko tayari tu kujitiisha Kwake, hilo ndilo jambo la kufanya.

⁸⁷ Mungu huchukua vitu rahisi. Wakati mwingine unaweza kufikiri kwamba wewe uko katika wachache hapa. Wachache, Mungu kwa kawaida huwa katika wachache. Lakini, ndugu, anapojitayarisha kuhama, Yeye huwatikisa walio wengi na walio wachache. Yeye ni Mungu. Anachukua vitu rahisi. Alipata wapi vitu vya kutengeneza ulimwengu navyo? Alinena na kusema, “Na iwe,” na ikawa.

⁸⁸ Alichukua mhubiri asiye na elimu, akamlea nyikani akila panzi na asali, karibu bila nguo yoyote aliyojifunika, ila kipande cha ngozi ya kondoo, na kutikisa maeneo hayo. Na jina lake lingali hai leo. “Mlitoka kwenda kuona nini?”

Mungu huchukua vitu rahisi.

⁸⁹ Alichukua mtu, wakati mmoja, ambaye karibu hakujuu hata ABC zake. Alichukua mtu wakati Wafilisti elfu moja walipomshambulia. Naye akaushika mfupa wa taya ya nyumbu, na kuchukua mfupa wa taya ya kawaida kutoka kinywani mwa nyumbu, na kuua watu elfu moja wenye silaha. Loo, huyo ndiye Mungu wetu, anayepanda mawimbi ya juu. Mfupa wa taya ya nyumbu, na kuua watu elfu.

⁹⁰ Mungu yule yule, wakati mmoja, wakati mtu mmoja mwenye majivuno makubwa ya Mfilisti aliposimama ng'ambo ya mto na kuyaasi majeshi ya Israeli, Mungu akamchukua maskini mvulana mdogo aliyekunjamana, aliyeonekana amekonda akiwa na kombeo rahisi mkononi mwake. Ee Mungu! Kombeo; kamba yenye ni-. . . imeunganishwa na ki—kipande cha ngozi. Maskini kombeo la zamani, kitu rahisi kama hicho, na kuua jitu na kulipiga jeshi hilo.

⁹¹ Mungu huchukua vitu rahisi. Haihitaji mambo makubwa. Inahitaji vitu rahisi vinavyotumika kwa usahihi. Sio vitu rahisi kabisa, lakini lazima itumike ipasavyo. Kila mtu aliyeishi nyikani hakuwa Yohana. Kila mtu aliyebeba kombeo hakuwa Daudi. Kila mtu aliyeokota mfupa wa taya ya nyumbu hakuwa Samsoni. Lakini inapotumiwa katika mikono iliyotiwa mafuta ya mtumishi wa Mungu!

⁹² Musa aliyaasi majeshi ya Israeli. . . au majeshi ya Misri, akiwa na kijiti kilichokauka mkononi mwake. Amina. Musa, siku moja mwoga, akiwa na Gershomu na Sipora, nyuma ya jangwa. Mara alipopakwa mafuta, kutoka kwenye kichaka kinachowaka moto, akiwa na fimbo kavu mkononi mwake, mke ameketi juu ya nyumbu, na mtoto mchanga nyongani mwake; umri wa miaka themanini, na masharubu yakipulizwa, wakashuka wakaingia Misri na kuchukua mamlaka. Rahisi, mzee mmoja, mwenye umri wa miaka themanini, akiwa na fimbo kavu ya mchungaji mkononi mwake, akayaasi majeshi yote ya ulimwengu, na akashinda, akatoka.

⁹³ Inategemea unachofanya. Sasa mnao unyenyekevu hapa. Mmepata Injili hapa Utica. Mnaweza kuwa, kama nilivyosema,

katika uchache. Lakini unakuja kusikia nini hapa? Unakuja kusema tu, “Ninaenda kanisani”? Je, unakuja tu kumsikiliza ndugu yetu mwenye neema? Hayo yote ni mazuri. Lakini hebu tufanye jambo zaidi ya hilo. Hebu tuje kumchukua Kristo. Hebu tuje, kuondoka hapa usiku wa leo pamoja Naye. Hebu tuende kukaidi kila kitu kibaya, tukatilie mbali. Mfupa wa taya, chochote kilicho mkononi mwako, pigana nacho. Mungu alitumia vitu rahisi, kwa mikono iliyotiwa upako. Una kazi rahisi; mji rahisi, mdogo; watu rahisi, wadogo; kanisa rahisi, dogo. Injili rahisi, lakini imetiwa mafuta. Mungu hivyo . . .

⁹⁴ Yehova mkuu mwenye nguvu Yule aliyenguruma kule, Yule aliyeziumba nyota na sayari za jua, Yule aliyeziumba ardhi kutokana na vitu visivyoonekana, akainena ikawepo, lakini, alipokuja kuwatembelea wanadamu, hakupanda magari ya dhahabu. Lakini alichagua kuja kwenye zi—zizi dogo ubavuni mwa kilima, na kuzaliwa Kwake kulikuwa kwenye hori ya ng’ombe. Mambo rahisi, lakini kutoka kwenye hori hiyo alikuja Imanueli. Mlitoka kwenda kuona nini? Ni nini kinachoikumba dunia leo? Je, ni kadi gani bora zaidi ya kupiga simu Marekani? Ni kadi gani kuu zaidi ya kupiga simu ulimwenguni? Je, ni jambo gani kuu kuliko nyakati zote na nyakati zote? Ni Uzima na Roho wa mtoto mchanga aliyezaliwa kwenye hori, katika zizi kando ya kilima.

⁹⁵ Mambo rahisi! Mambo rahisi! Imewekwa mkononi mwako, kanisa. Sasa chukua Upako na uutumie ipasavyo. Anaweza kuwa . . . watoto wote . . . Watoto wengi wamezaliwa kwenye mazizi. Watoto wengi wanaweza kuzaliwa kwenye hori. Lakini ni njia, wewe, unachofanya Nayo.

⁹⁶ Watu wengi wamesikia Injili ikihubiriwa. Graham ana ndugu waliosikia Injili ikihubiriwa. Nina ndugu waliosikia Injili ikihubiriwa. Ana ndugu, na wengine wana ndugu. Lakini ni kile unachofanya na Hiyo. Fanya. Hiyo ni ninii yako . . .

⁹⁷ Tunakaa na kubishania madhehebu yetu, tunapaswa kuwa wa kanisa gani, shirika gani. Hicho sicho kile ambacho Mungu hutuma wanadamu kusikia. Mungu huwatumia wateule Wake, watu Wake waliochaguliwa, kusikia Injili. “Injili imehubiriwa maskini.”

⁹⁸ Hapa wakati fulani uliopita, katika jimbo la Kentucky, juu milimani, hadithi inaendelea, ya mama mdogo, wa thamani, na watoto wapatao kumi, waliolazwa wakifa na ugonjwa huo mbaya wa kifua kikuu. Loo, alikuwa ametibiwa na kufanya kila kitu alichojua kufanya, lakini kijidudu hicho kilikuwa kinamuua. Ilikuwa ikimchukua. Alikuwa karibu kufa. Kati ya watoto hao kumi, bila shaka, aliwapenda, lakini hakukuwa na hata mmoja wao ila mmoja ambaye angefanya kazi. Hakuna hata mmoja wao ambaye angemsaidia. Alilala, akifa. Alilala kitandani. Hakuweza kuamka tena. Msichana

huyu mdogo, alifanya kazi yote ya kufua, huku dada zake wakienda kutembea, kwenda kwa majirani, kucheza. Na yeye akawapikia wengine. Wangukuwa nyumbani wakati wa chakula, kisha wakati wa kuosha vyombo ukiwadia, wangeondoka—wangeenda. Ilimbidi kufanya yote. Hakuna mtu mwingine aliyeachwa kuifanya. Hatimaye, kifo kilifika mlangoni, siku moja, na kumchukua mama yake.

⁹⁹ Ndipo yote yakatupwa kwake, kuwa mama wa watoto hawa wote. Maskini mtoto huyo akafanya kazi, na akafanya kazi, na akafanya kazi mpaka mikono yake midogo ikawa na sugu. Naye alifanya yote aliyoweza, kuwa mama, kuchukua mahali pa mama yake. Hatimaye, alifanya kazi kwa bidii sana, na hakupata chakula cha kutosha, pia, hata ugonjwa wa kutisha ukaushika mwili wake mdogo uliodhoofika. Hatimaye, akalala kitandani na alikuwa anakufa.

¹⁰⁰ Ilitokea kuwa, kote nchini, mwalimu wa shule ya Jumapili akaja kwa gari, akaingia ndani kumwona, akamwita kwa jina. Na yeye. . . Kasema, “Unaielewa kuwa ugonjwa wako ni mbaya?”

Naye akasema, “Ninaelewa kuwa ninakufa.”

¹⁰¹ Akasema, “Ndiyo kwanza nimwone daktari wako, naye akasema kwamba unakufa.”

Naye akasema, “Ndiyo. Hiyo ni sawa.”

¹⁰² Mbona, akasema, “Uko tayari kwa hili,” mwalimu mzuri akasema, “uko tayari kukutana na hii?”

Naye akasema, “Loo, ndiyo. Niko tayari kukutana na Bwana Yesu.”

¹⁰³ “Loo,” akasema, “hiyo ni nzuri sana. Vema, sasa, wewe ni wa dhehebu gani?”

¹⁰⁴ Akasema, “mimi si wa dhehebu lolote.” Akasema, “Nilifanya kazi kwa bidii sana hapa, hakuna mtu angenisaidia. Na,” kasema, “Mimi—mimi si mfuasi wa dhehebu lolote.”

¹⁰⁵ Akasema, “Mtoto!” Mwalimu mwema akasema, “Lazima uwe mfuasi wa dhehebu fulani.” Kasema, “Utaonyesha nini? Wewe ni wa dhehebu gani, utakapokuja mbele Zake?” Kasema, “Uta—utajishirikisha na kundi gani? Je, unaweza kumwambia kwamba wewe ni wa dhehebu gani? Unaweza kumwonyesha nini?”

¹⁰⁶ Maskini msichana huyo akiketi pale, akaitoa mikono yake midogo, yenye sugu kutoka chini ya kitanda. Kasema, “Nitamwonyesha tu mikono yangu. Ataelewa.” Nafikiri hiyo ni sawa.

¹⁰⁷ Kama tutamwonyesha tu, na yale ambayo tumefanya kwa yale aliyoweka mikononi mwetu. Hebu tufanye na yote yaliyo ndani yetu. “Mlitoka kwenda kuona nini?” Ataona nini ndani yako utakapokutana Naye siku hiyo? Ikiwa huna chochote cha

kumwonyesha, wakati kila kitu kipo cha kumwonyesha, liwazie, tunapoomba.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁰⁸ Je, kuna mtu angesema, “Niombee, Ndugu Branham, ninapoinua mkono wangu. Sasa ni—ninahisi kwamba ninataka kuchukua hii mikono yangu na kuiweka wakfu kwa Kristo, ili Yeye anitumie”? Inua mkono wako na useme, “Niombee.” Unapoinua mkono wako, sema, “Nitasalimisha yangu. Nataka.”

¹⁰⁹ Labda baadhi yenu Wakristo mngependa kusema, “Ni—ninatambua kwamba si—si—sijafanya tu mambo ambayo ninapaswa kufanya. Ninatambua nimekuwa mvivu sana. Hata hivyo, ninampenda Bwana Yesu. Na mimi—mimi nataka uniombee, Ndugu Branham. Nitainua mikono yangu.” Mungu akubariki. Hiyo ni nzuri.

¹¹⁰ “Ningependa kuwa na Yeye zaidi. Na—nampenda, na mimi—mimi nataka kukutana na Yeye Siku hiyo. Na ninapokifungua Kitabu, sitaki aseme, ‘Vema, uliweka jina lako kwenye Kitabu, lakini hukufanya lolote. Nataka kuleta nafsi. Ninataka kwenda nje na kufanya kitu.” Nataka kuomba. Mungu akubariki. Hiyo ni... Bwana akubariki, bwana.

¹¹¹ Hiyo ni kweli, mikono mingi, mikono mingi. Sasa, ninyi ambao mmeinua mikono yenu, kungekuwa na mwingine kabla tu hatujaomba? Mungu akubariki, msichana. Mungu akubariki, bwana. Na wewe hapa, ndugu yangu.

¹¹² Sasa ninapoomba, nanyi ombeni, pia. Unasema, “Bwana Yesu, Wewe—Wewe ulizungumza nami hapa, papa hapa nilipo. Sasa, kuanzia usiku huu na kuendelea, nitakutumikia Wewe. Ninatoka, kesho, kufanya onyesho. Ninatoka, si kujionyesha, lakini ninataka kila mtu amjue Yesu. Nami nitamfanyia jambo fulani. Nami nitajileta Kwako sasa hivi. Na Wewe unisamehe kwa jinsi ambavyo nimekuwa mzembe.”

¹¹³ Labda wewe si mhubiri, labda wewe si mwalimu wa shule ya Jumapili, lakini fanya jambo fulani. Wakati mwingine shuhudia tu kando ya barabara, nena na mtu fulani. Toka nje ukaimbe nyimbo huku ukifanya kazi kati ya wenye dhambi. Zungumza nao juu ya Bwana. Hivyo ndivyo unavyofanya. Hayo ndiyo yote Mungu anayohitaji. Fanya chochote kilicho mkononi mwako kufanya. Kifanya.

¹¹⁴ Sasa, Baba Mungu wa thamani, kwa unyenyekevu na utamu tunaleta sehemu hii ndogo ya ibada kwenye tamati, tukizileta zile mbegu zilizopandwa kila mahali, kwa kusomwa kwa Neno, kwamba uliuliza swali hilo la kutosha siku moja, “Mlitoka kwenda kuona nini?”

¹¹⁵ Kwa nini watu wanaenda kanisani? Ili tu ku—kujiunga na kanisa fulani au kuwa katika viwango vya kijamii vya dini? Ulienda kuona nini? Je, ulienda kuingia katika kanisa la jamii,

mahubiri ya kiakili? Au ulienda kutafuta amani? Je, ulienda kumtafuta Mwokozi? Mlitoka kwenda kuona nini?

¹¹⁶ Na, Baba Mungu, usiku wa leo, kupitia Neno Lako, kumekuwa na angalau watu kumi na watano hapa, au zaidi, ambao wameinua mikono yao. Kwa kuja usiku wa leo, wanataka kujitolea maisha yao. Labda waaminio Wakristo, lakini wanataka maisha yao yaonyeshe. Labda walihisi, kwa sababu hawakuitwa kwenye huduma, kuhubiri Neno ama kufundisha shule ya Jumapili, kwamba hawakuwa na sehemu. Lakini, Bwana, haijalishi ni rahisi jinsi gani, kutoka kwa mfupa wa taya hadi fimbo kavu, chochote kilicho mikononi mwetu, hebu tuonyeshe. Chochote kilicho mbele yetu, hebu tukifanye.

¹¹⁷ Mungu, ninaomba ya kwamba utayatakasa maisha yao, uyatie mafuta kwa Roho Mtakatifu. Na juhudi zao, kwa chochote kitakachokuwa, kuimba, kushuhudia, au kufanya jambo fulani, jalia iwe kwa heshima na utukufu Wako. Tujalie, Bwana.

¹¹⁸ Bariiki Ndugu yetu wa thamani na mwaminifu Graham, ambaye amesimama karibu na dawati hili kwa miaka mingi mirefu. Na kanisa dogo, kanisa dada la maskani, ninapoingia, usiku wa leo, na kuona kuna misalaba mitatu kwenye mi-mimbara, nami ninaona viti vya kanisa, na, hakika, Bwana, ni jamaa. Ni maskini, kanisa dada hapa mjini, kuangaza Nuru. Mungu, jalia likue na kuwa kanisa kuu. Tujalie, Bwana. Jalia Nuru ya Injili iangaze kutoka hapa, nje kupitia miji mingine. Jalia waje kutoka hapa wahubiri waliotiwa mafuta, watakaotoka katika hawa, kusanyiko hili, vijana hawa wanaoketi hapa, watakaopeleka Injili sehemu nyingine za ulimwengu.

¹¹⁹ Waimarishe na uwabariki mashemasi wake, na wadhamini wake, na washiriki wake wote. Jitwalie Mwenyewe utukufu, Bwana. Na usiku au mchana fulani, ama wakati wowote utakapokuwa, wakati huo mwito wa mwisho utakapotolewa nasi tuitwe kwenda Juu, tujalie tuje, tukileta nyara za thamani kuweka miguuni Pako, tukikupa Wewe kile tulichokushindia. Pia jalia nyenzo, ambazo Wewe uliziweka ndani ya mioyo yetu usiku wa leo, na tufanye kazi nazo, kwa yote yaliyo katika nguvu zetu; kuwabariki watu hawa, na kuwapa karama, karama za Roho, wapate kukufanyia kazi. Mimi sasa, kama mtumishi Wako, kwa agizo lililotolewa na Yesu Kristo, nawakabidhi mikononi mwa Mungu, kwa ajili ya huduma, katika Jina la Yesu. Amina.

¹²⁰ Kuna wimbo wa zamani, sijui kama dada yetu mdogo anaweza kuucheza, ama la, *Kuna Nafasi Kwenye Chemchemi*. Unaucheza? Sawa. Ni wangapi wanaoujua?

Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yangu.

¹²¹ Nakumbuka tulipokuwa tukiimba, na kushuka madhabahuni, kwa magoti yetu, na kuuimba, kule maskanini, miaka iliyopita. Na unajua, aina hii...Ninyi nyote mngali na hiyo dini huru hapa, kama tulivyokuwa nayo kule maskanini, ambapo bado unaweza kupiga makofi, umsifu Bwana, na kuwa na wakati mzuri.

¹²² Wananiambia, Ndugu Ruddell, hapa, ana maskani ya namna hiyo huko kwenye barabara kuu. Nitatoka na kumsikia moja ya siku hizi usiku. Alikuwa na wakati mbaya sana akisukumwa nje, lakini hatimaye anawachoma huko nje sasa. Mungu akubariki, Ndugu Ruddell.

¹²³ Vema, tupe sauti. [Mpiga kinanda anasema, "Uanzishe."—Mh.] Loo, Ndugu Graham, labda afadhali uwaanzishe sasa. Nataka kuuimba.

Nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako;
Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako.

¹²⁴ Unapenda hiyo? Sasa angalieni, ninyi Wamethodisti wote, na Wabaptisti, na Wapentekoste, na chochote mlichu. Hebu, tunapouimba huo tena, hebu tupeane mikono na mtu fulani, mbele yako, kando yako, pande zote mbili, na nyuma yako, wakati tunapouimba. Sasa njoo. Kuna nafasi kwa ajili yetu sote sasa.

Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako;
Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako.

Loo, nafasi, nafasi, kuna nafasi tele,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako;
Loo, nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako.

¹²⁵ Hivi hampendi huo? Unajua, Yakobo alichimba kisima. Na Wafilisti wakakimbia...kutoka kwacho, hivyo akakiita "uovu." Ndipo akachimba kisima kingine, nao Wafilisti wakamtorosha kutoka kwacho, kwa hiyo wakakiita "ugomvi." Akachimba kisima kingine, kisima cha tatu, akasema, "Kuna nafasi kwa ajili yetu sote."

¹²⁶ Na kwa hiyo Mungu alichimba kisima katika kanisa la Kilutheri, nao wakawafukuza wengine wote kutoka humo, Walutheri. Ndipo akachimba kisima kwenye kanisa la

Methodisti, chini ya utakaso. Walutheri walikuwa kuhesabiwa haki. Halafu, utakaso, akachimba kisima, na sasa wakafukuza wote kutoka kwake.

¹²⁷ Sasa amechimba kisima kingine. Hakina majina. Hapana, hakuna dhehebu. Ni Roho Mtakatifu aliye mwema, safi tu, na kuna nafasi kwa ajili yetu sote. Kwako wewe unayepanda ngamia mwenye nundu moja, ngamia wenye nundu mbili, ngamia wenye nundu tatu, chochote kile, kuna nafasi kwa ajili yetu sote.

Nafasi, nafasi, ndiyo, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako;
Loo, nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako.

¹²⁸ Je, hampendi nyimbo hizo za kale? Loo, ninazipenda tu. Na—nafikiri, baada ya kuhubiri, wakati mwingine ni kali sana na mbaya. Halafu tunapomaliza na hilo, unajua, inakusugua kabisa, basi unajisikia kama, umesafishwa tu kabisa, dhambi zako zote zimetoweka, zimeungamwa; unajisikia huru. Loo, basi ninajisikia kuimba tu. Sivyoye na nyinyi? Hiyo ni ibada. Paulo alisema, alipoimba, aliimba katika Roho. Ikiwa aliabudu, aliabudu katika Roho.

¹²⁹ Sijui kama dada anaweza kucheza hii, au la. Huenda nisiweze kuuimba. Lakini napenda wimbo huu. Ikiwa huwezi, ni sawa, dada.

Yesu, unihifadhi karibu na msalaba,
Kuna Chemchemi ya thamani,
Bure kwa wote, kijito cha uponyaji,
Kinatiririka kutoka Chemchemi ya Kalvari.

Msalabani, msalabani,
Uwe utukufu wangu milele;
Hata nafsi yangu iliyonyakuliwa itakapopata
Raha ng'ambo ya mto.

¹³⁰ Huupendi huo, mpenzi? Unajua, nilifanya hivyo tu ili kusikia sauti hizi nzuri za Utica zikiimba, mwajua. Tulikuwa na kinanda cha kale hapa juu, nawe ungekuwa na mikutano. Nyie watu wa Utica mnakumbuka hilo? Mnaenda na kuimba kwenye nyumba za mtu mwingine na kadhalika. Loo, ningependa kwenda kwa mmoja wao tena, niuimbe. Loo, jamani!

¹³¹ Hebu wazia, Mwokozi wetu wa thamani, hatuna budi kukutana Naye. Sijui lini; labda kabla ya asubuhi. Je, inaleta tofauti gani? Je, inaleta tofauti gani? Niambiieni. Nitafanya hivyo, hata hivyo, kwa hiyo hebu tu—tufarijike tu. Kuwa na imani. Mpende Yeye.

Yesu, unihifadhi karibu na msalaba,

Hapo Chemchemi ya thamani,
Bure kwa wote, uponyaji... (Inakutuliza tu,
unajua.)

Kinatiririka kutoka Chemchemi ya Kalvari.

Msalabani, msalabani,
Uwe utukufu wangu milele;
Mpaka... nafsi iliyonyakuliwa itapata
Raha ng'ambo ya mto.

Chini msalabani ambapo Mwokozi wangu
alifia,

Huko chini kwa ajili ya kutakaswa na dhambi
nililia;

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Loo, utukufu kwa Jina Lake, hilo Jina la
thamani!

Utukufu kwa Jina Lake!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Hebu tuinue mikono yetu sasa, tunapimba ubeti huu.

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu,

Yesu anakaa ndani vizuri sana,

Pale msalabani ambapo alinichukua;

Utukufu kwa Jina Lake!

Wakisema, utukufu kwa Jina Lake, Jina la
thamani!

Loo, utukufu kwa Jina Lake!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

¹³² Ni wangapi wanataka kwenda Mbinguni? Hakika, tunataka.
Ndiyo, bwana. Nataka kwenda. Niko njiani. Ninapenda tu kujua
kwamba ninao wanaume wenzangu na dada tukienda pamoja.
Ndiyo, bwana.

Njoo kwenye Chemchemi hii inayonisafisha,
Itupe maskini nafsi yako miguuni pa Mwokozi;

Loo, ingia ndani leo na ufanywe mkamilifu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa jina Lake la thamani!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa... .

Hiyo ni nzuri sana!

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu,

Yesu anakaa ndani vizuri sana,

Hapo msalabani ambapo alinichukua;

Utukufu kwa Jina Lake!

Loo, na utukufu kwa Jina Lake la thamani!

Utukufu kwa Jina Lake!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Njoo kwenye Chemchemi hii yenye utajiri na utamu sana;

Tupa roho yako maskini...miguu ya Mwokozi.

Je, ungependa kuja na kupiga magoti kwa muda?

...-siku, na kufanywa mkamilifu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Kuimba, utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!

Loo, utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Kuimba, utukufu kwa...

¹³³ Je, baadhi yenu mngependa kuja na kupiga magoti kuzunguka madhabahu sasa? Njoo na mvulana huyo mdogo. Njoo.

Utukufu kwa jina Lake la thamani!

Lo, huko kwa ninii yangu...

¹³⁴ Ndugu Beeler. Ndugu Beeler. Ndugu Beeler. Njoni hapa, ninyi ndugu. Ndugu Ruddell.

...Jina Lake!

Kuimba, utukufu kwa ninii Yake...

¹³⁵ Je, kunaweza kuwa na mtu mwingine ambaye angependa kuja na kupiga magoti? Njoni huku juu, kama mnataka kuweka maisha yenu wakfu kwa Mungu, wakati Roho Mtakatifu akiwa hapa.

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Njoo kwenye Chemchemi hii yenye utajiri na utamu sana;

Itupe maskini nafsi yako miguuni pa Mwokozi; Loo, jitumbukize leo hii, na ufanywe mkamilifu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Kuimba, utukufu kwa Jina Lake, hilo Jina la thamani!

Loo, utukufu kwa Jina Lake!

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Kuimba, utukufu kwa Jina Lake, Jina la thamani!

Utukufu kwa Jina Lake!

Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

Hivi hutakuja kwenye Chemchemi hii yenye
utajiri na utamu sana;

Itupe maskini roho yako . . .

¹³⁶ Hivi hutakuja, usiku wa leo? Piga magoti na kuomba. Mtu yeyote anayetaka kuja, njoo.

. . . ndani leo, na ufanywe mkamilifu;

Loo, utukufu kwa Jina Lake!

Kuimba, utukufu kwa Jina Lake, Jina la
thamani!

Utukufu kwa jina Lake la thamani!

Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Utukufu kwa Jina Lake!

¹³⁷ Loo, ni wakati mzuri jinsi gani! Loo, jinsi tulivyokuwa tukiimba wimbo huo wa zamani!

Itakuwa wakati mzuri kwako,

Wakati mzuri kwangu.

Ikiwa tutajitayarisha kukutana na Yesu

Mfalme wetu,

Utakuwa wakati mzuri jinsi gani.

¹³⁸ Je, hampendi huko kuabudu katika Roho? Naam, bwana. Inakulisha tu, kupitia nafsi yako. Haleluya! Haleluya!

¹³⁹ Nimefurahi sana kumwona Billy akijisikia hivyo. Ubariki moyo wake! Hebu tuimbe wimbo huu sasa.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,

Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,

Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini

ya mafuriko hayo,

Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

Sisi sote pamoja sasa. Tusaidie, Ndugu Graham.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,

Iliyotolewa kutoka kwenye mishipa wa

Imanueli,

Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya

mafuriko hayo,

Hupoteza waa lao lote la dhambi.

Hupoteza waa lao lote la dhambi,

Hupoteza waa lao lote la dhambi.

Kisha wenye dhambi hutumbukia chini ya

mafuriko hayo . . .

¹⁴⁰ Unajua, siwazi kamwe juu ya wimbo huo nisije nikafikiria hadithi ambayo niliambiwa wakati mmoja. Ilikuwa nje kwenye hifadhi huko Arizona. Kulikuwa na Tim Coy. Alikuwa kiongozi

kwa Wahindi, na kwa namna fulani mvulana mmishenari. Naye alikuwa amegeuzwa kule jangwani, na hangeweza kupata njia yake ya kutoka. Naye alikuwa amepanda farasi wake, ameishiwa na maji. Alikuwa amepotea kwa siku mbili au tatu mle ndani, hapo matumaini yote ya kwamba angetoka yalikuwa yamekwisha. Alisema alikuwa akishuhudia katika mkutano, na akasema ya kwamba ilionekana kuwa giza kuu kwake. Naye akakimbilia kwenye njia ya kulungu, huko nyikani, na kusema yule farasi aliyekuwa amempanda, kasema, alikuwa karibu amekwisha. Alikuwa . . . Naamini alisema jina lake lilikuwa ni Bess. Na akasema a—a—alimhurumia sana, alikuwa akitembea. Walikuwa na dhoruba kadhaa za mchanga, na pua zote zilijaa mchanga.

¹⁴¹ Na hiyo ndiyo sababu wanavaa hizo lesa. Wakati dhoruba ya mchanga inaendelea, wanaiweka juu ya uso wako. Nimepanda mara nyingi, na pumzi yangu ikiwa na unyevu, ingekuwa tu—ingetengeneza tu keki ngumu ya mchanga kuzunguka uso wako namna hiyo, ukipanda. Hilo vumbi, ng'ombe, unajua, na kadhalika, mbele yako. Na dhoruba za mchanga hulipeperusha hivyo.

¹⁴² Alisema alidhani ilikuwa karibu mwisho wa safari yake. Alikuwa akiumbayumba, yeye mwenyewe, farasi wake. Anaweza . . . Unaweza kuishi bila maji kwa muda mrefu kuliko farasi awezavyo. Kwa hivyo, alisema alikuwa akiumbayumba. Aliingia kwenye njia hii ya kulungu, na akasema alijisikia vizuri sana. Alianza kuteremka kwenye njia ya kulungu. Naye akapanda juu yake na akaanza kuendesha, na kusema alishuka kwenye hiyo njia kidogo. Kasema, loo, ilionekana kana kwamba kulikuwa na mamia ya kulungu wakishuka kwenye njia hiyo. Naye akawazia, “Vema, njia hiyo ya kulungu inaongoza kwenye maji, kwa hivyo nitapata maji.” Na akasema alianza na kupanda farasi wake.

¹⁴³ Akasema alifika mahali padogo ambapo watatu au wanne wakaelekea upande mmoja, na akasema farasi alitaka kuchukua njia hiyo. Akasema, “Loo, hapana, Bess. Huwezi kuchukua mkondo huo.” Akamshika kwa lijamu, na kumvuta huku namna *hii*. Kasema, “Nenda kwenye njia *hii*. Imewekwa alama bora. Hapa ndipo kulungu wote walikwenda kunywea.” Na akasema farasi akageuka, akaendelea tu kulia, kulia. Na akasema alikuwa amechangamka sana, alikuwa na njukuti za magurudumu, naye alimkata tu farasi huyo mpaka akasimama pale tu, akivuja damu. Na akasema asingeenda. Alitaka kuchukua njia hii ndogo.

¹⁴⁴ Unaona, hivyo ndivyo ilivyo kwa watu wengi. Wanapenda kufuata mkondo wa televisheni, nyota wa filamu, wachukue mkondo wa umaarufu, wawe mtu fulani mkubwa. Unaona? Hawaangalii njia hiyo ndogo.

Kuna njia kuu iendayo Mbinguni,

Kisichoonekana vizuri pale, kinjia, ndivyo wasemavyo;

Lakini ile pana inayoelekeza kwenye uharibifu Yote imepambwa na inang'aa kote njiani.

Wanasema kutakuwa na mkusanyiko mkubwa, Wakati makaoboi kama ndama wakiwa watasimama;

Watatiwa alama na waendeshaji wa Hukumu, Waliotumwa na wanajua kila chapa.

Mmeusikia huo wimbo.

Kwa hivyo nadhani ningekuwa mtoto wa mwaka mmoja aliyepotea,

Mtu tu ambaye amehukumiwa kufa,

Ingekatwa kwenye lundo na washamba,

Wakati Bosi wao wapanda farasi akipita.

¹⁴⁵ Alisema aliwazia hilo. Akasema, "Nilisikia kwamba..." Alimtazama, akawaza, "Kweli, Bess, ume—umenibeba umbali wote huu. Nilidhani nitakufa, nawe ukanibeba umbali huu. Na mara nyingi nimesikia kwamba farasi wana silika ya kujua mahali maji yalipo. Kwa hivyo ikiwa nimekuamini umbali huu, nitakuamini kupitia kinjia kisichoonekana vizuri."

¹⁴⁶ Hivyo ndivyo ninavyojisikia kuhusu Injili. Si kuilinganisha na farasi ambaye angekubeba, bali nimeamtumaini Bwana kupitia haya, maisha kama haya. Njia inapofifia, chini mwishoni mwa safari, ninataka kumwamini Yeye kuendelea. Unaona? Dini hii ya zamani iliniokoa huko nyuma, miaka thelathini iliyopita, imenibeba umbali huu wote. Ninapotembea katika bonde la uvuli wa mauti, ninataka tukio lili hili la moyoni. Nitaliamini basi.

¹⁴⁷ Akasema alimrukia, akaanza kuteremka. Hakuwa amekwenda sehemu yoyote, mpaka akaruka kichwa-mbele kwenye dimbwi kubwa la maji. Kasema alikuwa ndani ya maji hayo, akipigapiga tu, na akipiga mayowe kwa sauti kuu, akimtukuza Mungu. Aliosha pua zake, na kumrushia maji, na kupiga mayowe na kuendelea.

¹⁴⁸ Alisema alitoka tu majini, na kusema alisikia mtu akicheka. Akatazama ukingoni, lilikuwa ni kundi la watu waliosimama pale na gari kuu la kukokotwa lililofunikwa. Wote walikuwa wamelewa. Walikuwa kule kwenye karamu kubwa ya namna fulani, karamu ya kuwinda, ama kitu fulani. Na akasema wote walikuwa kwenye ulevi mkubwa. Na walionekana kumjua. Na akasema... Alisema, "Toka nje!"

Akasema, "Asante, wenzangu."

¹⁴⁹ Na akasema, "Nadhani una njaa." Akawaambia, alikuwa amepotea kwa siku kadhaa.

Kasema, "Naam."

¹⁵⁰ Akasema, “Vema, tuna mawindo hapa.” Hivyo wao . . . Akala mawindo. Akasema, “Sawa,” sema, “na wewe ni Jack, au Tim Coy, ki—kiongozi wa Kihindi?”

“Naam.”

¹⁵¹ Akasema, “Vema,” kasema, “kwa kuwa una mawindo mazuri, sasa,” kasema, “kinywaji kizuri kutoka kwa jagi hili kitakusaidia tu vizuri.” Alisema alimpa jagi.

¹⁵² Kasema, “Hapana, wavulana. Asante. Sinywi.” Kasema, alirudisha mguu wake juu, akapata maelekezo yake, na kuweka mguu wake kwenye kikuku, na kurudi juu ya farasi.

¹⁵³ Akasema jamaa mdogo aliyumbayumba, karibu nusu mlevi, akachukua moja ya bunduki hizo, Winchesters, na kutupa ganda ndani yake. Kasema, “Tazama, Tim! Ikiwa mawindo yetu yanatosha kukulisha, usijaribu kufikiria kuwa wewe ni mzuri sana kwamba huwezi kunywa viski yetu!” Unajua jinsi walevi walivyo.

¹⁵⁴ Akasema, “Angalieni, jamani,” akasema, “Sidhani kuwa mimi ni mzuri kupita kiasi kuinywa, lakini,” kasema, “Sinywi tu.” Akasema, “Mimi ni Mkristo.”

¹⁵⁵ Kasema, “Ah! Toka kwenye upuuzi huo.” Kasema, “Utachukua kinywaji hiki cha viski au nitapitisha risasi kwako.” Akijaribu kumwingiza kwake kwa hila.

¹⁵⁶ Kasema—kasema, “Subiri kidogo. Kabla ya kuitia risasi hiyo ndani yangu, ngoja nikupe hadithi yangu.” Akasema, “Nilizaliwa katika jimbo la Kentucky.” Kasema, “Baba yangu alikufa akiwa mlevi, amevaa viatu vyake.” Kasema, “Tuliishi katika nyumba ndogo ya zamani ya magogo. Ndipo asubuhi moja wakati jua lilipoanza kuchomoza, mchirizi kwenye sakafu ya kibanda kidogo, cha zamani, hata hakuwa na sa—sakafu ya mbao ndani yake.” Kasema, “Mama mmoja wa thamani alikuwa amelala akifa kwenye kitanda cha makapi.” Kasema, “Huyo alikuwa ni mama yangu.” Kasema, “Nilikuwa na umri wa miaka minane tu.” Tena akasema, “Aliniita kando ya kitanda, na kunikumbatia, akanibusu. Akasema, ‘Tim, ninakuacha. Baba yako alikufa, mlevi, akicheza kamari, alipigwa risasi akafa.’ Akasema, ‘Niahi, Tim, kabla sijafa, kwamba hutawahi kunywa pombe yako ya kwanza, au kujipumbaza na karata hizo.’” Alisema, “Nilipomuaga mama yangu kwa busu, nilimwahidi hivyo.” Akasema, “Sijawahi kunywa pombe tangu siku hiyo, kamwe, maishani mwangu.” Kasema, “Sasa ukitaka kupiga risasi, piga tu.”

¹⁵⁷ Na karibu wakati huo bunduki ilifyatuka. Jagi ya viski ikapasuka mkononi mwa mtu huyo. Mzee mdogo mwenye sura mbaya alitokeza kwenye genge. Alikuwa anatafutwa. Alikuwa jambazi. Akasema, “Hebu kidogo, Tim.” Akasema, “Ninatoka jimbo la Kentucky, pia.” Kasema, “Nilimuahidi mama yangu sitakunywa pombe kamwe.” Akasema, “Nimekuwa nikisimama

hapa nikingojea hadi wakajisikia vizuri na kulewa kabisa, basi nilikuwa ninaenda kuwagonga, kila mmoja kichwani, na kuchukua pesa walizokuwa nazo.” Wawindaji! Akasema, “Hiyo ndiyo niliyokuwa nimesimamia hapa. Lakini niliposikia ushuhuda wako, Kitu fulani kilinena na moyo wangu.” Kasema, “Ninasikitika nilivunja ahadi yangu kwa mama.” Akasema, “Lakini bastola yangu ilipopiga mwangwi kupitia magenge makubwa ya Mbinguni, alinisikia nikitia sahihi ahadi, ‘Sitakunywa tena, tangu wakati huu na kuendelea.’” Akasema, “Huu ndio wakati wangu wa kuacha.” Mara nyingi nimefikiria hivyo.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu, (haijalishi kama ungepita kwenye njia hii ya zamani iliyofifia),
 Iliyotolewa kutoka kwenye mishipa ya Imanueli
 Ambapo wenye dhambi hutumbukia chini ya mafuriko,
 Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

Hivyo ndivyo unavyofanya.

Tumbukia chini ya mafuriko,
 Hupoteza waa lao lote la dhambi.

¹⁵⁸ Huu hapa wimbo mwingine ninaoupenda sana. Nina hakika nyote mnaujua.

Imani yangu inakutazamia Wewe,
 Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
 Mwokozi wa Kiungu;
 Sasa nisikie ninapoomba,
 Ondolea mbali hatia yangu yote,
 Na uniruhusu tangu siku hii
 Niwe Wako kabisa.

¹⁵⁹ Mnaujua? Mnaupenda? Hebu tuuimbe, basi. Hebu tusimame tunapouimba.

Imani yangu inakutazamia Wewe,
 Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
 Mwokozi wa Kiungu;
 Sasa nisikie ninapoomba,
 Ondolea mbali hatia yangu yote,
 Loo nijalie tangu siku hii
 Niwe Wako kabisa!
 Ninapopitia kwenye mzingile wa maisha,
 Na huzuni imenizunguka,
 Uwe Kiongozi wangu;
 Amuru giza ligeuke . . .

Ndugu Graham. 

59-1001 Mlitoka Kwenda Kuona nini?
Glad Tidings Tabernacle
Utica, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org